## Suala kuu la 10

## Tohara? Hapana!

*Bilan alitumwa na mwalimu wake ampelekee tabuleti yake, aliyoisahau darasani. Ulikuwa ni wakati wa mapumziko, kwa hivyo wanafunzi walikuwa nje wakicheza.*

*Tabuleti ile haikuwa imezimwa. Bilan alishangazwa na kuwapo kwa mafaili mengi kwenye kiwambo cha tabuleti ile. Anwani za mafaili yale zilimvutia. Bilan alipata hamu ya kusoma baadhi ya mafaili yale. Alilifungua faili ambalo mwalimu wao alikuwa amewatajia. Lilikuwa ni faili lenye matini kuhusu hatari za tohara kwa watoto wa kike.*

*Moja kwa moja, Bilan alianza kusoma habari zile.*

### Tohara? Hapana!

Dora alibaki darasani wakati wa mapumziko mafupi. Wenzake wote walikimbia uwanjani kwenda kucheza. Wengine walienda msalani.

"Una nini, Dora? Kwa nini huendi kucheza na wenzako?" Bi. Rehema aliuliza aliporudi darasani kuchukua simu yake iliyokuwa ikichaji.

Dora alishindwa kumjibu, akaanza kulia. Bi. Rehema aliketi karibu na Dora na kumfuta machozi.

"Tafadhali, niambie kinachokusumbua. Niamini, sitamwambia yeyote. Itabaki kuwa siri yetu," Bi. Rehema alimsihi.

"Ninaweza kukuamini, mwalimu?" Dora aliuliza.

"Unaweza kuniamini kwa lolote. Nitakusaidia kwa kila hali," Bi. Rehema alimwambia.

"Ni jamaa zangu … Wanataka kunitia tohara. Naogopa sana, mwalimu. Nisaidie," Dora alisema kwa wasiwasi.

"Nimekuelewa, Dora. Usijali. Hilo ni suala dogo sana kwetu. Kuwa na imani kwamba uko kwenye mikono salama. Nitakusaidia," Bi. Rehema alimhakikishia.



Kimeidhinishwa na KICD

Bi. Rehema alimweleza Dora kuwa utamaduni wa kuwapasha tohara wasichana ulikuwa umepitwa na wakati. Alimjulisha kuwa ilikuwa ni hatia pia kwa yeyote kumwoza mtoto wake kabla hajatimiza umri unaofaa. Alimjuza kuwa angepeleka ombi kwa mwalimu mkuu ambaye bila shaka angelifikisha kwa chifu. Kwa kufanya hivyo, Dora angepata hifadhi katika makao ya watoto ili asije akadhulumiwa.

Kwa ruhusa ya mwalimu mkuu, Bi. Rehema aliwapigia simu wazazi wa Dola na kuwaomba wafike shuleni ili wazungumze. Walipofika, aliwaeleza kuhusu madhara ya tohara kwa mtoto msichana. Aliwaeleza pia kuwa wangehukumiwa kisheria ikiwa wangeendeleza unyama ule.

Wazazi wa Dora waliingiwa na hofu. Walimwomba msamaha Bi. Rehema. Waliahidi kuwa wangefanya kila juhudi kumlinda mtoto wao.

*Bilan alipomaliza kusoma, alishtuka kumwona mwalimu wake kando yake. Aliingiwa na woga, akawa anataka kuomba msamaha.*

*"Ninaona nilisahau kuifunga tabuleti yangu. Mbona unasoma habari zisizokuhusu? Ndiyo, nimekosea, lakini kwa nini hujazingatia hatua za kiusalama nilizowafunza kuhusu vifaa vya kidijitali?"*

*"Nisamehe, mwalimu. Sitarudia," aliomba radhi.*

*"Nimekusamehe, lakini siku nyingine, ukipata kifaa hakijafungwa, jua kuwa ni wajibu wako kukifunga. Usianze kusoma mafaili."*